# SHERIA YA KUTOZA KODI NA KUFUTA BAADHI YA KODI NA TOZO NA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI ZINAZOHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA UMMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Marekebisho ya sheria mbali mbali.

**SEHEMU YA PILI**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTARATIBU NA USIMAMIZI WA KODI, NAM. 7 YA MWAKA 2009**

3. Kusomwa.
4. Marekebisho ya kifungu cha 5.
5. Kuongezwa kifungu kipya cha 53C.
6. Marekebisho ya kifungu cha 54A.
7. Kuongezwa kifungu kipya cha 68A.

**SEHEMU YA TATU**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA ADA YA HUDUMA YA BANDARI, NAM. 2 YA MWAKA 1999**

8. Kusomwa.
9. Marekebisho ya kifungu cha 4.

**SEHEMU YA NNE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA, NAM. 12 YA MWAKA 2016**

10. Kusomwa.

11. Marekebisho ya kifungu cha 133C.

**SEHEMU YA TANO**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA KUKUZA NA KULINDA UWEKEZAJI ZANZIBAR, NAM. 14 YA MWAKA 2018**

12. Kusomwa.

13. Marekebisho ya kifungu cha 31.

14. Kuongezwa kifungu kipya cha 31A.

15. Marekebisho ya kifungu cha 47.

**SEHEMU YA SITA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI, NAM. 4 YA MWAKA 1998**

16. Kusomwa.

17. Marekebisho ya kifungu cha 2.

18. Marekebisho ya kifungu cha 5.

**SHERIA NAM. 4 YA 2022**

**NIMESAINI**

**{DKT. HUSSEIN ALI MWINYI}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

25.06. ......................................................, **2022**

# SHERIA YA KUTOZA KODI NA KUFUTA BAADHI YA KODI NA TOZO NA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI ZINAZOHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA UMMA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

*Jina fupi na kuanza kutumika.*

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Mapato ya Umma), 2022 na itaanza kutumika mara tu baada ya kutiwa saini na Rais.

*Marekebisho ya sheria mbali mbali.*

**2.** Sheria zilizotajwa katika sehemu mbali mbali za Sheria hii zinarekebishwa kwa namna zinavyoelezwa katika sehemu husika.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA UTARATIBU NA USIMAMIZI WA KODI, NAM. 7 YA MWAKA 2009

*Kusomwa.*

**3.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Utaratibu na Usimamizi wa Kodi, Nam. 7 ya Mwaka 2009 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**4.** Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongezwa vifungu vidogo vipya vya (6) na (7) mara tu baada ya kifungu kidogo cha (5) kama ifuatavyo:

"(6) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki, mtu atatakiwa kusajiliwa katika Kodi ya Ongezeko la Thamani, ikiwa mtu anatoa huduma za kitaalamu kama huduma hizo za kitaalamu zitatolewa na mtu huyo, mjumbe au mwajiriwa wa mtu huyo.

(7) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, maneno "huduma za kitaalamu" maana yake ni huduma zinazotolewa na mtu ama aliyepewa leseni kama mtoaji huduma hizo na bodi yoyote ya kitaalamu inayotambulika au asiyepewa leseni na itajumuisha huduma nyengine au shughuli za kibiashara zinazojitegemea ikijumuisha ushauri elekezi, sheria, usanifu wa majengo, uhandisi, usimamizi, uhasibu, ukaguzi, utabibu, usanii, utafiti, maonesho ya sanaa, michezo, maonesho, huduma binafsi za ulinzi, uchunguzi binafsi na ushauri elekezi katika kada tofauti au burudani yoyote inayofanywa au kutolewa isipokuwa zinazofanywa kwa malipo kwa mujibu wa mkataba wa ajira".

(b) kukipa nambari upya kifungu kidogo cha (6) kuwa kifungu kidogo cha (8) na kifungu kidogo cha (7) kuwa kifungu kidogo cha (9).

Kuongezwa kifungu kipya cha 53C.

**5.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 53C mara baada ya kifungu cha 53B kama ifuatavyo:

"Makubaliano ya bei kabla

**53C.**-(1) Kamishna anaweza, kwa ombi kutoka kwa mlipa kodi au kwa jitihada zake mwenyewe na baada ya kupata idhini ya Waziri, kuingia katika Makubaliano ya Bei ya Kabla na mlipa kodi kwa kuweka vigezo vya kutambua bei kwa baadhi ya miamala ya baadae inayofanywa na mlipa kodi kwa kipindi maalum.

(2) Iwapo Kamishna ataingia katika Makubaliano ya Bei ya Kabla na mlipa kodi, bei ya miamala iliyotambuliwa katika makubaliano itakuwa ni msingi wa thamani ya muamala wa kodi kwa kipindi ambacho Makubaliano ya Bei ya Kabla ni halali.

(3) Makubaliano yaliyoingiwa ya Bei ya Kabla chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, yatatumika katika miamala iliyoainishwa katika makubaliano.

(4) Makubaliano yaliyoingiwa ya Bei ya Kabla chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, yatakuwa halali kwa kipindi kisichozidi miaka miwili kuanzia tarehe yalipofungwa ikizingatiwa kwamba mkataba huo unaweza kupitiwa katika muda wowote kulingana na mazingira yatakayoainishwa na Kamishna katika Miongozo.

(5) Kamishna anaweza, kwa notisi ya maandishi na baada ya kupata idhini ya Waziri, kufuta Makubaliano ya Bei ya Kabla na mlipa kodi, ikiwa:

(a) mlipa kodi ameshindwa kufuata sharti lolote muhimu la makubaliano;

(b) kumekuwa na uvunjifu mkubwa wa moja au zaidi kati ya dhana za msingi zilizomo katika makubaliano;

(c) kumekuwa na mabadiliko ya sheria za kodi ambazo zina mahusiano makubwa na makubaliano;

(d) makubaliano yaliingiwa kwa njia ya udanganyifu, kimakosa au kutokufanywa kwa jambo lolote na mlipa kodi.

(6) Usitishwaji wa Makubaliano ya Bei ya Kabla chini ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki utaanza kutumika:

(a) endapo kwa kifungu kidogo cha (5)(a) na (c) kutoka tarehe iliyoainishwa na Kamishna kwa notisi ya usitishwaji;

(b) endapo kwa kifungu kidogo cha (5)(b) kutoka tarehe ulipotokea uvunjwaji mkubwa;

(c) endapo kwa kifungu kidogo cha (5)(d) kutoka tarehe iliyofungwa mkataba".

Marekebisho ya kifungu cha 54A.

**6**-(a). Kifungu cha 54A cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa kifungu kidogo cha (2).

(b) Kuvipa nambari upya vifungu vidogo vilivyobakia kwa mpangilio wake.

Kuongezwa kifungu kipya cha 68A.

**7.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 68A mara baada ya kifungu cha 68 kama ifuatavyo:

"Zawadi kwa kutoa taarifa

**68A.**-(1) Kamishna anaweza kutoa zawadi kwa mtu yeyote kwa kutoa taarifa zitakazopelekea kutambua au kugomboa kodi au ushuru ambao haujakisiwa ikizingatiwa kwamba kifungu hiki hakitatumika kwa ofisa au mtu yeyote anayefanya kazi kwa niaba ya Bodi.

(2) Zawadi itakayotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itatolewa kwa mujibu wa miongozo iliyoidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi".

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA ADA YA HUDUMA YA BANDARI, NAM. 2 YA MWAKA 1999

Kusomwa.

**8.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ada ya Huduma ya Bandari, Nam. 2 ya Mwaka 1999 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**9.** Kifungu cha 4 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kufutwa aya ya (a) na kuwekwa badala yake aya mpya ya (a) kama ifuatavyo:

"(a) mtoto yeyote asiyehitajika kuwa na tiketi kama itakavyoainishwa na Mamlaka ya Usimamizi".

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA FEDHA ZA UMMA, NAM. 12 YA MWAKA 2016

Kusomwa.

**10.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma, Nam. 12 ya Mwaka 2016 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 133C.

**11.** Kifungu cha 133C cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa kifungu kidogo cha (1) na kuwekwa badala yake kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"(1) Kwa kuzingatia masharti ya sheria husika au sheria nyengine yoyote, Waziri anaweza kusamehe yote kamili au sehemu ya kodi, ushuru, tozo, ada au malipo mengine kwa Amri iliyochapishwa katika Gazeti Rasmi endapo ni mradi na kwa kutaarifiwa endapo si mradi".

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA KUKUZA NA KULINDA UWEKEZAJI ZANZIBAR, NAM. 14 YA MWAKA 2018

Kusomwa.

**12.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar, Nam. 14 ya Mwaka 2018 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 31.

**13.** Kifungu cha 31 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongezwa kifungu kidogo kipya cha (5) mara baada ya kifungu kidogo cha (4) kama ifuatavyo:

"(5) Kwa madhumuni ya kukuza uwekezaji, Waziri, kwa kushauriana na Waziri anayehusika, anaweza kujadiliana na kuamua vivutio visivyokuwa vya kodi; ikizingatiwa kuwa makubaliano yoyote yanayohusiana na vivutio vya kodi yatafanywa kwa kushauriana na Waziri anayehusika na Fedha".

(b) kukipa nambari upya kifungu kidogo cha (5) kuwa kifungu kidogo cha (6).

Kuongezwa kifungu kipya cha 31A.

**14.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 31A mara baada ya kifungu cha 31 kama ifuatavyo:

"Matumizi mabaya ya Msamaha wa Kodi.

**31A.**-(1) Mwekezaji ambaye amepewa msamaha wa kodi chini ya Sheria hii na akautumia vibaya msamaha, ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika:

(a) kulipa kodi ambayo ingeweza kulipwa iwapo msamaha usingetolewa; na

(b) kulipa adhabu ya asilimia hamsini ya kodi ambayo ingeweza kulipwa iwapo msamaha wa kodi usingetolewa.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, hakutakuwa na msamaha mwengine wa kodi utakaotolewa kwa mwekezaji huyo".

Marekebisho ya kifungu cha 47.

**15.** Kifungu cha 47 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa aya ya (e) na kuwekwa badala yake aya mpya ya (e) kama ifuatavyo:

"(e) atatumia vibaya fursa au vivutio visivyokuwa vya kodi vinavyotolewa chini ya Sheria hii".

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI, NAM. 4 YA MWAKA 1998

Kusomwa.

**16.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Nam. 4 ya Mwaka 1998 ambapo katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**17.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongezwa ufafanuzi wa maneno yafuatayo katika mpangilio wa kiherufi:

"soko la kimtandao" maana yake ni jukwaa ambalo linawezesha mahusiano ya moja kwa moja baina ya muuzaji na mnunuzi wa bidhaa au huduma kupitia njia za kielektroniki;

"huduma ya kielektroniki" inajumuisha usambazaji au muamala unaofanywa kupitia mawasiliano ya mtandao, mawasiliano ya simu au kupitia masoko ya mtandao, utoaji wa upakuzi wa maudhui, vitabu vya kielektroniki, vyombo vya habari vya kulipia, huduma za utoaji maudhui kwa mtandao ikijumuisha maonesho katika televisheni, filamu, muziki, podikasti, programu na mifumo yake ikijumuisha mfumo wa programu, viunganishi vya programu, vichujio vya tovuti na ngome ya kimtandao; usimamizi wa data za kielektroniki ikijumuisha usimamizi wa tovuti, kubadilishana mafaili mtandaoni na huduma za uhifadhi wa data mtandaoni; muziki na michezo ya kimtandao; mashine taftishi, dawati la huduma za usaidizi za kimtandao linalojiendesha, tiketi za matukio ya moja kwa moja, masomo ya kimtandao, vyombo vya habari vya kimtandao; huduma zinazounganisha msambazaji na mpokeaji ikijumuisha huduma za usafiri au majukwaa ya kimtandao na huduma nyengine yoyote inayotolewa kupitia soko la kimtandao na jukwaa jengine lolote la kidijitali au huduma;

"bidhaa" maana yake ni aina yoyote ya mali inayohamishika na isiyohamishika, isipokuwa hisa, dhamana au fedha;

"huduma" inajumuisha huduma za mawasiliano ya simu, huduma za kielektroniki au kitu chochote ambacho si bidhaa au fedha ikijumuisha lakini haimalizii kwa:

(a) utoaji wa taarifa au ushauri;

(b) ruzuku, utoaji wa kazi, kufuta au kurudisha haki;

(c) kupelekea upatikanaji wa huduma, fursa au faida;

(d) kuingia katika makubaliano ya kuzuia au kuvumilia jambo, hali au kufanya jambo; na

(e) kutoa, kuhaulisha au kurudisha leseni, kibali, cheti, makubaliano, uidhinishaji au haki inayofanana;

"Huduma ya mawasiliano" maana yake ni aina ya huduma inayotolewa na mtu au kampuni kwa njia ya usambazaji, utoaji, upokeaji wa alama au viashiria vya alama, maandishi, picha na sauti au taarifa zenye kufahamika za aina yoyote, kwa njia ya waya au njia yoyote ya mifumo ambayo inajumuisha:

(a) sauti, mawasiliano ya sauti, huduma za taarifa, huduma za ujumbe wa sauti, huduma za ujumbe wa video, miito ya redio na njia nyengine za mawasiliano ya kielektroniki zinazokubalika;

(b) huduma za simu za mezani zinazojumuisha utoaji wa matumizi ya mitandao ya simu inayotumia na isiyotumia mitambo ya kuwashia na kuzimia huduma kwa kuunganisha usafirishaji na utoaji wa sauti na picha na huduma za simu zinazoingia na kutoka za kitaifa na kimataifa;

(c) huduma za simu za mkononi zinazojumuisha upatikanaji na matumizi ya mitandao inayotumia na isiyotumia mitambo kwa usambazaji na usafirishaji wa sauti, taarifa, huduma, picha na huduma zinazoongezeka thamani kwa huduma za mawasiliano zinazoingia na kutoka za kitaifa na kimataifa;

(d) huduma za mawasiliano zinazojumuisha maeneo ya utoaji wa huduma ya matumizi ya nyaya, mkonga au matumizi yasiyo ya waya na teknolojia nyengine za kuanzisha, kumalizia au kupitisha mawasiliano, utozaji wa uunganishaji, upatikanaji, kusitisha simu za ndani na kimataifa kwa utozaji wa matumizi ikijumuisha nguzo, utoaji wa ukodishwaji inayowaunganisha kupata huduma au njia za muunganisho wa taarifa au njia za ujumbe kwa njia ya hawala;

(e) utoaji wa huduma za usimamizi wa simu kwa malipo inajumuisha huduma za kusubiri simu, kuhamisha simu, kutambua mpiga simu, upigaji wa simu nyingi, kuonekana simu, marejesho ya kupiga simu, uzuiaji wa simu, kurejesha moja kwa moja simu iliyopigwa, kujibu simu, mawasiliano ya simu, huduma tofauti za simu na huduma za mikutano kwa simu;

(f) huduma za mitandao binafsi inayojumuisha utoaji wa mawasiliano kwa njia ya waya au isiyotumia waya, mkonga na teknolojia nyengine yoyote ya mawasiliano ya kielektroniki inayounganisha baina ya vituo kwa matumizi makhsusi ya mteja;

(g) huduma za usambazaji wa taarifa zinajumuisha upatikanaji wa huduma kwa njia ya nyaya au zisizokuwa za nyaya na huduma nyengine makhususi zilizoandaliwa kwa ufanisi wa usambazaji wa taarifa;

(h) mawasiliano kupitia kidughushi (facsimile), sauti, nukushi, simu ya maandishi na huduma za maandishi na huduma nyengine za kimawasiliano ya kielektroniki; na

(i) huduma nyengine yoyote inayoweza kuongezwa kila baada ya muda na watoaji wa huduma za mawasiliano ya simu".

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**18.** Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongezwa kifungu kidogo kipya cha (7) mara baada ya kifungu kidogo cha (6) kama ifuatavyo:

"(7) Katika utaratibu wa kifedha, taasisi ya fedha inayotoa gharama pamoja na faida, unaoruhusiwa na Benki Kuu ya Tanzania ambayo inamuwezesha mtu kupata bidhaa au mali kutoka kwa muuzaji kupitia taasisi ya fedha:

(a) taasisi ya fedha itachukuliwa kuwa haijanunua au kuuza bidhaa chini ya utaratibu huu wa kifedha;

(b) mteja atachukuliwa kuwa amenunua bidhaa kutoka kwa muuzaji kwa kuzingatia kiwango sawa na kilicholipwa na taasisi ya fedha moja kwa moja kwa muuzaji;

(c) faida yoyote inayolipwa au inayopaswa kulipwa kwa taasisi ya fedha na mteja itachukuliwa kuwa malipo kuhusiana na huduma ya kifedha yenye msamaha iliyotolewa na taasisi ya fedha;

(b) kukipa nambari upya kifungu kidogo cha (7) kuwa kifungu kidogo cha (8).

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 22 Juni, 2022.

..............................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***